

Kulipia bili

Karatasi la uhakika wa muongozo wa pesa zako

Bili ni nini?

Bili ni gharama ya kutumia kitu, kwa mfano, maji, gesi, umeme, simu ya nyumbani, simu ya mkono na tuvuti. Wewe unaweza kupokea bili kwa kila huduma uliyoitumia.

Nitapata bili kwa matumizi ya aina gani?

Utapata bili kwa ajili ya maji, gesi, umeme, simu ya nyumbani, simu ya mkono na tuvuti.

Naweza kuzilipia bili vipi?

Kunazo njia tofauti za kulipia bili. Hii inafanuliwa kwenye maelezo ya bili yako, kwa mfano, unaweza kutumia akaunti yako ya benki kupitia simu au kwenye tuvuti. Wewe unaweza kulipia mwenye kwenye afisi ya posta au kwa kutumia cheki hundii au money order. Kama unapata mapato kutoka Centrelink unaweza kulipa kutumia huduma ya bure inayoitwa Centrepay. Wewe pia unaweza tumia huduma ya direct debit ambayo wewe unaweza kuanzisha kupitia wanaokutolea huduma.

Na kama siwezikama kulipasawezi kulipa bili?

- ▶ Pigia kampuni haraka unavyoweza.
- ▶ Unaweza kupata usaidizi kutoka Mshauri wa Kifedha bila malipo.
- ▶ Usiipuuze shida ya kutoweza kulipa bili.

Kumbuka

- ▶ Bili ni gharama ya kutumia kitu, kwa mfano, maji, gesi, umeme, simu ya nyumbani, simu ya mkono na tuvuti.
- ▶ Kila mtu anawajibika kulipa bili.

Jinsi ya kupata maelezo zaidi

Kwa usaidizi na shida za kulipa bili, wasiliana na Mshauri wa Kifedha bila malipo kwenye simu 1800 007 007 au wasiliana na wanaokutolea huduma kwenye nambari iliyoandikwa kwenye bili.

Kwa maelezo zaidi kuhusu Washauri wa Kifedha, tembelea tuvuti ya MoneySmart, www.moneysmart.gov.au, au pigia 1300 300 630.

Kwa maelezo zaidi kuhusu Ombudsman wa Kiwanda cha mawasiliano kwa kutumia huduma za simu, tuvuti, nk, tembelea tuvuti ya www.tio.com.au, au pigia simu 1800 062 058.

Kwa huduma za Ombudsman wa nguvu za umeme pamoja na Ombudsman wa maji tembelea tuvuti ya MoneySmart, www.moneysmart.gov.au, na uzitafute bili za manufaa.



Pata usaidizi bila malipo kutoka Mshauri wa Kifedha

Reda na Heba wanazo shida za kulipa bili zao. Hawajuia nini kinahitajika kulipwa na lini.

Wanakumbuka kuwa walipowasili mara ya kwanza hapa Australia walikwenda kwenye ukumbi wa jiji na kusikiliza maelezo kutoka mfanyakazi wa makazi. Mfanyakazi wa makazi aliwaeleza kikundi baadhi ya huduma za mtaani zinazopatikana kwao kupitia watoaji huduma. Kitu kimoja waliambiwa ni kwamba wanaweza kuwasiliana na Mshauri wa Kifedha Bure ili kupata usaidizi.

Reda na Heba wanaweza kupigia watoaji huduma na kuwaeleza shida zao au wanaweza kupata usaidizi kutoka kwa Mshauri wa Kifedha bila malipo. Waliambia kupata usaidizi kutoka Mshauri wa Kifedha kwa sababu hawakujua nini kusema au kuuliza kila mtoaji huduma au kuuliza kila mtoaji huduma kwenye simu.

Jina la Mshauri wa Kifedha ni Mary na kwanza alieleza nini wanachofanya washauri wa kifedha na jinsi wanavyoweza kusaidia. Kitu moja wanachofanya ni kusaidia watu kupangilia taarifa ya gharama au mpangoo wa kulipa pesa wanazodaiwa. Reda na Heba wanajihisi afadhali sasa kwa kuwa wameshaongea na kufaidika na ushauri wa Mary.

Mary husaidi Reda na Heba kwa kuwasiliana sawia na huduma inayotoa pamoja na kupangilia mpango wa kulipa ambao unatoshea kwenye taarifa ya gharama yao. Siku iliyofuatia Mary alimpigia Reda na Heba ili kuwaeleza nini yeye ameshafanya na kuwauliza waandike chini lini bili zao zote zinafaa kulipwa na kiasi cha pesa wanachohitaji kulipa kwa kila moja. Yeye alipendekeza kutumia kalenda na kuweka alama kwenye tarehe bili inahitajika kulipwa.

Reda na Heba wanamshukuru Mary kwa usaidizi wake. Baada ya simu wanaandika chini kwenye kalenda ni bili ngani zinahitajika kulipwa, wakati zinahitajika kulipwa na pesa ngapi wanafaa kulipa.

This page has been left intentionally blank.